Viongozi wakutana kuadhimisha mwaka mmoja wa Ushirikiano na Serikali Wazi

Baada ya kuzinduliwa na Rais Obama wa Marekani na mwenzake Rousseff wa Brazil pamoja na watendaji mbalimbali wa asasi za kiraia, akiwemo Mkuu wa Twaweza, Rakesh Rajani, Mpango wa kimataifa wa kuendesha shughuli za Serikali kwa Uwazi (unaofahamika kama OGP) unalenga kuzisaidia SSerikali kuibua njia mpya za kuwashirikisha raia na kutumia ueelewa na ujuzi wao ili kutoa maamuzi makini (katika masuala yanayowahusu).

Katika kipindi cha mwaka mmoja tu, OGP imekua kutoka nchi nane waanzilishi hadi nchi 57 zinazoshiriki. Serikali za Tanzania na Kenya nazo zimekubali na kudhamiria kuwa wazi zaidi kwa wananchi wao. Kwa sasa, Tanzania ni mwanachama katika Kamati Tendaji inayoongoza maendeleo na mwelekeo wa OGP.

Serikali Wazi nchini Tanzania
Tanzania imekwishawasilisha Mpango Kazi wake wa Serikali yenye Uwazi wa mwaka 2012 – 2013. [http://bit.ly/SayVD5] Dhamira hizo zimeelezwa kwa ufupi hapa chini, na Mpango umetoa kipaumbele kwa upatikanaji wa taarifa kuwa ni mhimili muhimu kwa Tanzania kuelekea kwenye SSerikali yenye Uwazi.

- Nyaraka za bajeti kwa wananchi zinatayarishwa na kuwekwa kwenye tovuti mbalimbali
- Jukwaa la pamoja kati ya Serikali na Asasi za Kiraia (CSOs) ili kusimamia utekelezwaji wa dhamira za OGP limeanzishwa
- Mfumo wa uainishaji vituo vya maji kwenye mtandao kwa ajili ya Serikali za Mitaa (LGAs)
- Uwekaji taarifa kwenye mtandao kuhusu dawa zilizoagizwa na kupokelewa
- Uchapishaji wa taarifa za upelekaji fedha za ruzuku kwa kila mwanafunzi zinazotolewa

Kuna mafanikio yamefikiwa katika utekelezaji , hasa katika uchapishaji wa bajeti za wananchi mtandaoni na kiwango cha uwazi katika namna Bunge linavyoendesha shughuli zake. Hata hivyo, Serikali na Asasi za kiraia nchini Tanzania, bila kusahau vyombo vya habari, vitahitajika kuendelea kutoa msukumo wa kuendeleza uwazi.

OGP inahimiza mbinu ya utawala makini zaidi, yenye ufanisi na yenye kuleta tija zaidi.
Uwazi na Uwajibikaji – teknolojia mpya zinawapa wananchi njia mpya za kupata taarifa, na OGP inakuza na kuboresha hili zaidi. Serikali iliyo wazi zaidi ina maana ya Serikali inayowajibika, kwani inawapa watu mamlaka na nafasi zaidi katika masuala ya umma.
Ushiriki – pale wananchi wanapoweza kusimamia maendeleo na kushiriki kwa njia yenye tija zaidi katika kutoa uamuzi unaothiri maisha yao, wanaweza kuleta matokeo chanya katika maendeleo ya nchi yao.
Ushirika – Asasi za kiraia, wafanyabiashara na Serikali – wamekuwa kitu kimoja na sawa katika Serikali wazi. Kila upande una wajibu tofauti, na unatoa changamoto kwa pande nyingine ili kuchagiza mabadiliko.
Uchumi – SSerikali wazi inaweza kuzalisha mapato kwa ajili ya biashara na kuzisaidia Serikali kufanya maamuzi makini na yenye ufanisi zaidi, kuokoa fedha na kuleta thamani kubwa ya matumizi ya fedha.

Katika maadhimisho ya mwaka mmoja, Tanzania iliwakilishwa na Waziri Chikawe, ambaye ndiye kiongozi wa OGP nchini, na Mkuu wa Twaweza, Rakesh Rajani, ambaye alitoa hotuba ya kufunga. Akieleza kwamba OGP ingeweza kutoa mwanya kama Serikali zitajipanga kuwajibika kwa raia, Rajani

alisisitiza *"[Tunahitaji] kuibua njia mpya ya ushirikiano katika kuendesha Serikali, njia ambayo haihimizi tu kutoa amri (na maelelezo) bali inayoweka mazingira ya Serikali na raia kuungana na kutatua matatizo ya jamii nzima."*

Maadhimisho ya mwaka mmoja ya OGP yalifanyika jijini New York wakati Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa ukiendelea. Maadhimisho hayo ya kwanza yalihudhuriwa na watu wengi maarufu na kupokewa kwa shauku kubwa ambapo hotuba za viongozi mbalimbali wa OGP na wawakilishi wa taasisi muhimu za kiraia zilitolewa. Tukio hilo pia lilishuhudia kuzinduliwa kwa Mfumo Huru wa Utoaji Taarifa (IRM) – unaoundwa na jopo la a watu maarufu na wataalamu wa sera katika ngazi ya kimataifa walio na uzoefu mkubwa – ambao watafuatilia maendeleo na kuhakikisha kuna uwajibikaji mkubwa wa Serikali zinazoshiriki kwenye mpango wa OGP. Wakati wa tukio hilo, Uingereza na Indonesia zilichaguliwa kushika kiti cha Uenyekiti wa OGP, pamoja na mwenyekiti mwenza wa asasi za kiraia Warren Krafchik kutoka International Budget Partnership (Ushirika wa Kimataifa katika masuala ya Bajeti).

Katika mwaka wake wa kwanza, OGP imeonesha kwamba duniani kote kuna nia ya kuzifanya Serikali ziwe wazi zaidi. Lakini, kwa mujibu wa washiriki wengi waliohudhuria maadhimisho hayo ya kwanza, wakati wa kutoa maazimio ulikuwa umekwisha, na sasa ilikuwa ni wakati wa vitendo na uwajibikaji. Wananchi ulimwenguni kotewanatazama yanayoendelea, ni suala la muda tu ambapo itadhihirika kama kweli OGP imeweze kufikia matarajio.

--- Mwisho ---

Taarifa-takwimu kuhusu OGP zinapatikana kwa ajili ya uchapishaji wa makala na habari kuhusu maadhimisho haya ya kwanza. Pakua taarifa hizo hapa
http://blog.opengovpartnership.org/2012/09/open-government-partnership-first-year-infographic/

Vidokezo kwa Wahariri

- Ushirikiano na Serikali yenye Uwazi (OGP) ulizinduliwa mwezi Septemba 2011 na wenyeviti wenza wawili wa kwanza, Rais Obama wa Marekeni, na Fousseff wa Brazil, walioazimia nia kwa pamoja na nchi washiriki kuzifanya tawala zao ziwe wazi na zinazowajibika zaidi.
- Katika mkutano wake wa kwanza wa mwaka, uliofanyika katika jiji la Brasilia mwezi Aprili, wawakilishi kutoka Tanzania waliungana na wenzao kutoka pande mbalimbali duniani, na kubadilishana uzoefu na maarifa kuhusu dira na mipango ya kitaifa kwa ajili ya kufungua milango ya Serikali kwa wananchi. Kwa pamoja, Serikali zinazoshiriki kwenye OGP ziliweka dhamira tofauti zipatazo 300.
- Nchi zinazoshiriki (ambazo zimefikia 57) zinawakilisha takribani watu bilioni mbili, sawa na asilimia 30 ya idadi ya watu wote ulimwenguni.
- Kwa taarifa zaidi kuhusu OGP, ikiwa ni pamoja na orodha ya nchi zinazoshiriki, tembelea www.opengovernmentpartnership.org
- Kwa taarifa zaidi kuhusu dhamira zilizowekwa na Tanzania na tarehe za utekelezaji, tembelea www.opengovpartnership.org/countries/tanzaniana http://blog.opengovpartnership.org/2012/09/tanzania-ogp-update/